

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA
AFRIKA MASHARIKI

Simu: +255-26- 2323201-7
Nukushi: +255-26-2323208
Barua pepe: nje@nje.go.tz
Tovuti: www.foreign.go.tz



Jengo la LAPF Ghorofa ya 6,
Barabara ya Makole,
S.L.P 2933,
DODOMA.

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

FURSA ZA UFADHILI WA MAFUNZO KWA WATUMISHI WA UMMA

Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki imepokea fursa za ufadhili wa masomo ya muda mrefu katika sekta ya miundombinu chini ya program itwayo "Global Infrastructure Development Scholarship Program (GIDSP) kutoka Jamhuri ya Korea.

Mafunzo haya ambayo ni kwa ajili ya Watumishi wa Umma yatafanyika katika Chuo Kikuu cha Seoul (UOS) nchini Korea kuanzia mwezi Agosti 2018 hadi Desemba 2019.

Waombaji wa mafunzo haya wanatakiwa kutuma maombi yao moja kwa moja kwenye Chuo Kikuu cha Seoul (UOS). Maelezo ya ziada kuhusu mafunzo haya na namna ya kutuma maombi yanapatikana kupitia tovuti ya <http://isus.uos.ac.kr> au maombi yatumwe kwa barua pepe ifuatayo: mipd@uos.ac.kr. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 18 Mei, 2018.

Mafunzo haya yanaratibiwa na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Imetolewa na:
Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali,
Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki,
Dar es Salaam
03 Mei, 2018

